



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI
(Barua zote zilandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Kumb.Na. MDC/C.50/29/7

Tarehe:04/10/2022

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, anawatangazia wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, nafasi ya Uenyekiti wa Bodi ya Ajira Tangazo hili ni kwa Mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 (127) na (128) 2. Bodi ya Ajira katika Mamkala ya Serikali za Mitaa inashughulika na masuala ya Ajira na uthibitishaji wa watumishi kazini kulingana na Sheria, Kanuni na taratibu zinazoongoza Utumishi wa Umma.

SIFA ZA MWOBAJI

Mwombaji wa nafasi hii anapaswa kuwa na sifa zifuatazo kulingana na Kanuni ya 128 (4) (a) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003:

- (a) Awe ni mkazi wa eneo la Halmashauri ya Wilaya ya Moshi
- (b) Asiwe na majukumu yatakayomfanya asipatikane/asihudhurie kwenye vikao vya Bodi ya Ajira.
- (c) Awe na Elimu ya kidato cha Nne/Sita na taaluma kwenye maeneo yafuatayo:-
 - Utawala
 - Rasilimali Watu
 - Sheria

MSHAHARA

Nafasi ya Uenyekiti wa Bodi ya Ajira haina mshahara wowote.

Mwenyekiti wa Bodi, Katibu na wajumbe wa Bodi ya Ajira hulipwa posho ya kikao kulingana na nyaraka mbalimbali za Serikali. Kwa sasa posho ya kikao inalipwa kwa mujibu wa Waraka wa posho za vikao maalum.

MKATABA WA KAZI

Kwa Mujibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003 130 (1&2) atakayefanikiwa kupata nafasi hii na ikiwa hakutatokea tatizo lolote, atahudumu kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia Oktoba 2022 – Septemba 2025.

JINSI YA KUTUMA

Maombi yatumwe kwa njia ya posta kwa kutumia anwani ifuatayo:

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P. 3003,
MOSHI.

MWISHO WA KUPOKEA MAOMBI:-

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 17/10/2022 saa 9:30 Alasiri siku ya Jumatatu.

TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:



KASTORI G. MSIGALA
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
MOSHI